# Ombi la Mabadiliko – Agizo la Kiidara

## Petition for Modification – Administrative Order

KUMB: ) NAMBA YA KESI:
Mlezi )
)
)
Mzazi wa Kisheria )

**Maelekezo**

Ispokuwa kwa saini yako, tafadhali chapisha majibu yote. Tumia wino wa bluu au mweusi tu.

WAC 388-14A-3925 inakutaka:

1. Uandike kiasi (kipya) cha msaada wa mtoto kinachopendekezwa.
2. Ueleze sababu ya ombi lako la mabadiliko.
3. Utie saini fomu.

Huna budi kukamilisha na kurudisha kwa DCS nyaraka zilizoorodheshwa kwenye ukurasa wa 2 wa fomu hii.

ZINGATIA: Kama hutakamilisha hatua zote zinazotakiwa katika fomu hii, Hakimu wa Sheria ya Kiidara (ALJ) anaweza akafuta ombi hili.

**Ombi**

Mimi, __________________________________________________, naiomba Ofisi ya Usikilizwa wa kesi wa Kiidara ikiongoze Kitengo cha Msaada wa Watoto (DCS) na watu waliotajwa hapo juu wajitokeze na kueleza kwa nini agizo langu la kiidara la msaada wa watoto halitakiwi kubadilishwa. Agizo langu la kiidara la msaada wa watoto liliandikwa tarehe __________________________________________________.

Ninaamini kiasi cha sasa cha msaada wa watoto kwa kesi hii kinatakiwa kuwa $_______________ kwa mwezi.

Ninaamini kiasi cha sasa cha msaada kinatakiwa kurekebishwa kwa sababu:

__________________________________________________

__________________________________________________

__________________________________________________

__________________________________________________

__________________________________________________

__________________________________________________

__________________________________________________

**Tazama ukurasa wa 2 na wa 3 kwa mahitaji ya ziada na sehemu ya saini yako.**

**Kukiri**

Nafahamu kwamba:

1. DCS itakataa ombi hili kama halina vigezo vya kubadilisha agizo vilivyomo katika RCW 74.20A.059.
2. Kama agizo langu kwa sasa halina mambo haya, DCS itamwomba ALJ aingize mambo haya kwenye agizo langu akimtaka kila mzazi kutoa ulinzi wa bima ya afya ya watoto kama ulinzi upo sasa au utakuwepo kupitia ajira au chama na malipo ya bima ya afya hayavuki asilimia 25 ya wajibu wa msaada wa msingi wa mzazi. DCS itazingatia sharti hili kuwa limetosheleza ikiwa watoto wanastahiki Huduma za Afya za Kihindi. DCS inaweza ikatekeleza wajibu huu katika hali fulani. Mzazi aliyewajibishwa hana budi kutoa ushahidi wa ulinzi wa watoto unaoweza kufikiwa kwa DCS na kwa mzazi mwengine ndani ya siku 20 za tarehe ambayo liliandikwa agizo la mwisho la msaada wa mtoto. Kama mzazi aliyewajibishwa hatatoa ushahidi wa ulinzi, mzazi aliyewajibishwa anaweza kutakiwa kutosheleza wajibu ili kutoa bima ya afya kwa kufanya moja ya yafuatayo, kwa mpangilio wa kipaumbele:
    a. Kutoa au kupata ulinzi wa bima ya afya kwa kupitia ajira au chama cha mzazi aliyewajibishwa kwa gharama isiyozidi asilimia 25 ya wajibu wa msingi wa mzazi aliyewajibishwa wa msaada wa mtoto.
    b. Kuchangia kiasi chenye uwiano cha mzazi aliyewajibishwa cha malipo ya mwezi kinacholipwa na mzazi mwengine kwa ajili ya ulinzi wa bima ya afya ya watoto waliotajwa kwenye agizo la msaada, kisizidi asilimia 25 ya wajibu wa msingi wa mzazi aliyewajibishwa wa msaada wa mtoto.
3. Sina budi kuomba kiasi maalumu cha msaada wa mtoto, kutoa sababu za kuomba marekebisho, na kutia saini fomu hii. Kama sitafanya hivyo, DCS haitafanyia kazi ombi langu.
4. Sina budi kuandika nyaraka zifuatazo nikiwa na DCS.
    a. Ombi hili lililojazwa.
    b. Karatasi za ***Ratiba ya Msaada wa Watoto ya Jimbo la Washington*** zilizojazwa.
    c. **Kama mimi ni mzazi wa watoto,** ushahidi wa kipato (kumbukumbu ya malipo, ripoti ya kodi, n.nk.)
5. Sina budi kutuma kwa barua nyaraka zilizopo hapo juu kwenda anwani ifuatayo au kuzifikisha mimi mwenyewe kwenye ofisi ya DCS ambayo imeshika kesi yangu.

    DIVISION OF CHILD SUPPORT<br>PO BOX 11520<br>TACOMA WA 98411-5520
6. Kama sitakabidhi kwa DCS nyaraka zilizopo hapo juu, Hakimu wa Sheria ya Kiidara (ALJ) anaweza akafuta ombi langu.
7. Kama nitabadili anwani yangu sina budi kuifahamisha DCS.
8. Sina budi kuifahamisha DCS kuhusu mabadiliko yoyote katika ulinzi wa bima ya afya ya watoto wangu.
9. DCS hainiwakilishi mimi au mtu mwengine kwenye agizo la msaada wa mtoto wangu katika hatua hii.
10. Kama sitahudhuria na kushiriki katika usikilizwaji wa kesi uliopangwa, ALJ anaweza akafuta ombi langu.
11. Kama mtu mwengine wa kwenye agizo langu hatahudhuria na kushiriki katika usikilizwaji wa kesi uliopangwa, ALJ anaweza:
    a. Kutoa idhini yoyote iliyoombwa na DCS au mtu aliyejitokeza katika kesi bila taarifa zaidi.
    b. Kuamuru kiasi cha msaada ambacho ni cha juu au cha chini kuliko kiasi kilichopendekezwa kwenye ombi hili.

## Taarifa kwa Wazazi Wote Wawili

ALJ anaweza:

1. Kuwaamuru wazazi wote wawili kutoa bima ya afya ya watoto kama ulinzi upo sasa au utakuwepo kupitia ajira au chama na malipo ya bima ya afya hayavuki asilimia 25 ya wajibu wa msingi wa wazazi wa msaada wa watoto.
2. Kuwaamuru wazazi wote wawili kulipa kiasi chenye uwiano cha matumizi ya matibabu yasiyokuwa na bima, yakiwemo malipo binafsi, malipo ya madai, na sehemu yoyote ya kiasi chenye uwiano cha malipo ya bima ya matibabu yasiyotekelezwa kupitia huduma ya ***Notice of Support Owed.***
3. Kuamuru kwamba kama mzazi ambaye ameamuriwa kutoa ulinzi wa bima ya afya kwa ajili ya watoto hatoi ushahidi wa ulinzi unaoweza kufikiwa, DCS inaweza kufanya moja ya yafuatayo, yameorodheshwa kwa mpangilio wa kipaumbele:
    a. Kutuma taarifa kwa mwajiri au chama ikimtaka mwajiri au chama kuwasajili watoto kwenye mpango wa bima ya afya kama inavyoelezwa katika RCW 28.18.170.

    b. Kuihudumia taarifa ya mzazi aliyewajibishwa ikimtaka mzazi alipe kiasi chake chenye uwiano cha malipo ya mwezi kinacholipwa na mzazi mwengine kwa ajili ya watoto, kisivuke asilimia 25 ya wajibu wa msingi wa msaada wa watoto wa mzazi aliyewajibishwa.
4. Kuamuru kwamba kama mzazi aliyewajibishwa atashindwa kuwasajili watoto kwenye ulinzi wa bima ya afya unaoweza kufikiwa, au ulinzi uliopo kupitia mwajiri wa mzazi au chama, DCS inaweza ikatekeleza wajibu wa msaada wa matibabu wa mzazi aliyewajibishwa kama inavyoelezwa katika RCW 26.18.170.

## Tamko

Natamka wazi chini ya adhabu ya kusema uwongo, chini ya sheria za jimbo la Washington, kwamba yaliyotajwa hapo juu ni kweli na sahihi.

## Unalazimika kusaini fomu hii

| | |
|---|---|
| ______________________ TAREHE | ______________________ SAINI YANGU |
| ______________________ SANDUKU LA BARUA AU ANWANI YA MTAA | ______________________ JINA LA MWANASHERIA WANGU AU MWAKILISHI |
| ______________________ MJI WANGU   JIMBO   MSIMBO | ______________________ ANWANI YA MWANASHERIA WANGU AU MWAKILISHI |
| (      ) NAMBA YA SIMU YA NYUMBANI \| (      ) NAMBA YA SIMU YA MKONONI | ______________________ MJI WA MWANASHERIA WANGU AU MWAKILISHI, JIMBO, MSIMBO |
| (      ) NAMBA YA SIMU YA KAZINI \| (      ) NAMBA YA SIMU YA UJUMBE | (      ) NAMBA YA SIMU YA MWANASHERIA WANGU AU MWAKILISHI |
| (      ) NAMBA YA FAKSI | |
| ______________________ SAA NZURI ZA KUNIPIGIA SIMU | |
| ______________________ NAMBARI NINAYOPENDA KUITUMIA KWA USIKILIZWAJI WA KESI | |

Hakuna mtu kwa sababu ya mbari, rangi, asili ya uraia, imani, dini, jinsia, umri, au ulemavu, atabaguliwa katika ajira, huduma, au sehemu yoyote ya shughuli za programu. Fomu hii inapatikana katika miundo mingine kulingana na ombi.